

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 5 Aprili, 2022**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA  
YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Kwaya ya Bunge iliimba Wimbo wa Taifa na  
Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mhe. Shamsi Vuai Nahodha

*(Hapa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahonda Aliapa Kiapo  
cha Uaminifu)*

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilete kwenu taarifa yangu ambayo inatolewa kutoka katika Kanuni yetu ya 39(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Sita wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada mitatu ya Sheria ambayo ni hii ifuatayo:

Kwanza; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendment Bill, 2022*). Pili; ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utakatishaji Fedha wa mwaka 2022 (*The Anti-Money Laundering Amendments Bill, 2022*). Tatu; Muswada wa Sheria ya Nyongeza ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022 (*The Supplementary Appropriation for Financial Year 2021-2022, Bill*).

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa tayari Miswada hiyo mitatu imeshapata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na kuwa sheria za nchi zinazoitwa sasa ya kwanza inaitwa, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Sheria Na. 1 ya mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendment Act No. 1 of 2022*); Sheria ya pili inaitwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utakatishaji Fedha Sheria Na. 2 ya mwaka 2022 (*The Anti- Money Laundering Amendment Acts, No. 2 of 2022*); Sheria ya tatu ni Sheria ya Nyongeza ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali Sheria Na. 3 ya mwaka 2022 (*The Supplementary Appropriation for Financial Year 2021/2022 Act No. 3 of 2022*).

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo kazi mliyoifanya Mheshimiwa Rais pia ameshaifanya kwa sehemu yake na imekamilika.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu wote nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Shamsi Vuai na nimkaribishe tena Bungeni. Pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wenyeveiti wa Kamati na Makamu Wenyeveiti kwa kazi nzuri mliyoifanya katika kipindi hiki ambacho Bunge lilikuwa linaendelea na Kamati lakini mlifanya ziara za kuangalia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022 pia kuangalia mapendekezo ya Serikali kwa mwaka unaokuja wa fedha. Kwa hiyo, ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu mliowapa Wenyeveiti na pia ninawashukuru kwa kazi nzuri, ninaamini katika kipindi hiki cha Bunge tutaendelea na hiyo kazi ya kuwawakilisha wananchi wetu kwa maana ya kuishauri Serikali, kuisimamia Serikali na kutunga sheria pale panapohitajika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo machache tutaendelea na ratiba yetu. Katibu!

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

### **HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Niwakumbushe utaratibu

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tulioelekezana jana kuhusu maswali ya nyongeza yawe mafupi.

Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero sasa aulize swali lake.

Na. 1

### **Ujenzi wa Soko Ifakara**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, ni lini wananchi wa Ifakara watapewa fedha za ujenzi wa Soko la Halmashauri ya Mji wa Ifakara ambao umesuasua kwa muda sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Jimbo la Kilombero kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara kuwa na Soko la Kisasa ili kuboresha mazingira ya wafanyabishara wa Mji wa Ifakara na kuongeza mapato ya Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Mji wa Ifakara iliandaa na kuwasilisha Serikali Kuu andiko la mradi wa kimkakati wa ujenzi wa soko hilo kwa gharama ya shilingi bilioni 14.3 ambalo halikukidhi vigezo. Hivyo, Halmashauri ya Mji wa Ifakara inahimizwa kuweka kipaumbele na kutenga fedha kwenye bajeti yao ili kukamilisha andiko la mradi huo ambalo litawezesha kutafuta fedha za kutekeleza mradi huo.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri sasa Mheshimiwa Abubakari Asenga swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kwa kuzingatia maelekezo yako ya maswali ya nyongeza yawe mafupi, nakushukuru sana swali langu kuwa la kwanza katika Bunge lako hili la kwanza ikiwa Simba imeshafanya yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wakati Simba ikifanya yao tayari *Yanga Sport Club* ikiwa inaongoza ligi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa naomba kuuliza maswali yangu mafupi madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuzingatia majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba tumekosa fedha kutokana na ripoti ya wataalam wetu au andiko la wataalam wetu kutokukidhi vigezo. Je, Mheshimiwa Waziri anatumakikishia kwamba ataweza kutupatia wataalam ili tuandike upya andiko hili?

Swali la pili, wananchi wa Mji wa Ifakara wanateseka sana kutokana na soko hasa msimu huu wa mvua. Je, Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa TAMISEMI atakuwa tayari katika Bunge hili kutafuta hata siku moja kutembelea soko hili na kuzungumza na wananchi wa Mji wa Ifakara?

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge huo ni mfano mzuri wa maswali mafupi ya nyongeza lakini yale maelezo ya mwanzo hayatakiwi kuwepo ukipewa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Silinde naomba upite hapa mbele tutarejesha utaratibu wa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kujibu kutokea hapa mbele lakini ukishakuja hapa ukishajibu hayo ya nyongeza unakaa hapo mpaka wale wengine pia wakuulize maswali tumalize ndiyo unaenda kukaa.

Mheshimiwa Naibu Waziri karibu kwa majibu.  
*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Jimbo la Kilombero kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza aliuliza kwamba kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunaweza kuwapatia wataalam. Tuko tayari kuwapatia wataalam ambao watashirikiana na Halmashauri ya Mji wa Ifakara kuhakikisha wanakamilisha andiko lao, kwa hiyo hilo tuko tayari.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu kwenda Ifakara. Mheshimiwa Mbunge mimi niko tayari hususani wakati wa *weekend* tunaweza tukaongozana kwenda kushuhudia hiyo kero ya wananchi katika eneo lako. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge wa Sumve Mheshimiwa Kasalali Mageni swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuwa hali ilivyo Kilombero inafanana kabisa na ilivyo katika Jimbo la Sumve katika eneo la Bungulwa ambapo Halmashauri tumeshaleta andiko la kujenga soko la kisasa katika mnada wa Bungulwa.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuleta pesa ili mradi huu muhimu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ufanyike?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasalali, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, anasema Halmashauri yake imeshaleta andiko katika ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa sasa anachohitaji tu ni kwamba fedha sasa itolewe kwa ajili ya soko hilo. Mimi tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaenda kupitia hilo andiko na kuangalia namna bora ambayo tunaweza tukatafuta fedha kuhakikisha kwamba tunaleta katika Halmashauri yake.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo *commitment* ya Serikali, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

Na. 2

### **Kujenga Barabara ya Ivuna hadi Chole – Songwe**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA K.n.y. MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Ivuna hadi Chole ili kurahisisha mawasiliano kati ya Wilaya ya Momba na Songwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ivuna hadi Chole yenye urefu wa kilomita 18.5 ni barabara muhimu iliyopo Wilaya ya Momba ambayo inaungainisha barabara ya

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Muheza hadi Isanzu yenye urefu wa kilomita 12 katika Wilaya ya Songwe. Ili kuunganisha Wilaya hizi mbili jumla ya kilometa 30.50 zinatakiwa kufanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali itatenga jumla ya Shilingi Milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa daraja lenye urefu wa mita 200 katika barabara ya Ivuna – Chole Wilaya ya Momba na kwa upande wa Wilaya ya Songwe Shilingi Milioni 100 kwa ajili ya kufanya matengenezo yenye urefu wa kilomita 3 katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara katika barabara hii yenye urefu wa kilometa 30.5 kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Changamoto iliyopo Mkoa wa Songwe inafanana kabisa na changamoto iliyopo Mkoa wa Dodoma katika Wilaya ya Chamwino na Wilaya ya Chemba.

Ni lini Serikali itajenga barabara ya kutokea Itiso, Zajirwa mpaka Kimaha kwa maana ya Kata ya Kimaha kuunganisha na Wilaya ya Chemba?

Pili, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutokea Kimaha – Soya – Msada mpaka Wilaya ya Kondoa? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kunti Majala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameanisha hapa hizi barabara ikiwemo Itiso – Kimaha na nyingine Kimaha – Soya na maeneo yote ambayo ameyainisha kwamba, anataka kujua tu *commitment* ya Serikali ni lini itajenga barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, ninaamini katika bajeti ya fedha ya mwaka unaokuja ziko sehemu za hizi barabara alizoiainisha tumezitengea fedha na nyingine tutaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha barabara hizi zote zinapitika kwa wakati wote. Kwa hiyo, hilo ndio jibu la Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kuhusiana na barabara hiyo, ombi langu ni kwamba, Serikali haioni haja katika kipindi ambacho tunasubiri matengenezo ya hiyo barabara tupate daraja la dharura ambalo limefanya kusiwe na mawasiliano kabisa ya wananchi hawa? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Jimbo la Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ni kwamba, katika jibu letu tumeshaweka *commitment* ya kutenga fedha shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo. Bahati nzuri mwaka wa fedha huu unaoanza, ambacho naweza nikamhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Momba ni kwamba, daraja hilo litajengwa katika mwaka wa fedha unaokuja,

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kabla ya msimu wa mvua kuanza. Kwa hiyo, hiyo ndio *commitment* ya Serikali. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara ya kutoka Iringa Mjini kwenda Kilolo ambayo ilikuwa ni kilometa 33, lakini inapita Jimbo la Kalenga kutoka Ipogolo kwenda Kilolo, lini itajengwa kwa sababu imekuwa ni muda mrefu haijajengwa? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anahitaji tu *commitment* ya Serikali ya ujenzi wa barabara kilometa 33 kutokea Iringa kwenda Kilolo ambayo inapitia Kalenga ambayo muda mrefu haijajengewa. Ni kwamba barabara hii tumekuwa tukitengea fedha za matengenezo; na kwa sababu, Serikali inazingatia umuhimu wa hayo maeneo, na ninafahamu katika mwaka unaokuja kuna fedha imetengwa kwa ajili ya kuhakikisha yale maeneo korofi yote yanatengenezwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza kwamba, hii barabara ambayo inazunguka *fence* ya kwa Waziri Mkuu; *fence* ile imepakwa rangi nyeupe, lakini ina vumbi na kipindi cha mvua ina tope. Ni lini mtajenga kwa kiwango cha lami ili kuweza kutunza ile *fence* nzuri inayozunguka kwa Waziri Mkuu yenye rangi nyeupe? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa David Ernest Silinde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge anachozungumza kwamba, hii barabara ya nyuma inayozunguka *fence* ya Waziri Mkuu ni ya vumbi na tumekuwa tukiitengeneza kwa kiwango cha changarawe. Kwa hiyo, sasa anahitaji *commitment* ya Serikali ya kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, niwaagize *TARURA* Mkoa waende wakafanye tathmini ya ujenzi wa kiwango cha lami. Wakishakamilisha hiyo tathmini, basi watuletee Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutajua wapi ambapo tutatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega.

Na. 3

### **Kukamilisha Kituo cha Afya Kiloleli – Busega**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha Kituo cha Afya Kiloleli pamoja na kupeleka Vifaa kwenye Hospitali ya Wilaya Busega?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe, Mbunge wa Jimbo la Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Kiloleli kilipandishwa hadhi kutoka Zahanati kuwa Kituo cha Afya mwaka 2016. Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya Kituo hicho ambapo jumla ya shilingi milioni 57 zilipelekwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kujenga Wodi ya Wazazi na ujenzi wa Jengo la stoo ya dawa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 shilingi milioni 90 zimepelekwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi, kwa maana ya *three in one*, ujenzi ambao upo katika hatua ya msingi. Mpango wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga shilingi milioni 500 katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kupitia Bohari Kuu ya Dawa. Tayari baadhi ya vifaa tiba vimeshapelekwa kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Busega. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Kituo hiki cha Afya Kiloleli kinahudumia zaidi ya Kata tatu kwa maana ya Kiloleli, Nyaruhande pamoja na Rubugu, lakini kina kituo cha afya kimoja: Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa wodi ya wanawake, watoto pamoja na wanaume ili kukidhi mahitaji ya kituo cha afya hiki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Waziri yuko tayari kutembelea Kituo cha Afya Kiloleli ili kuona mahitaji ya wananchi hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, alichoomba Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, pamoja na kwamba kituo hiki cha afya kinafanya kazi, ameomba tu tuongeze fedha kwa ajili ya wodi tatu ili kuhakikisha kwamba kiwe *full* kwenye matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu sasa hivi tumekuwa tukipata fedha karibu kila mwezi na zile fedha tumekuwa tukizielekeza kule, kwa hiyo, fedha nyingine tutatenga kwa ajili ya kuhakikisha tunapata wodi tatu katika kituo hiki ili kiwe *full* katika matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, la pili, ameomba kwenda kutembelea. Najua ni rafiki yangu na anaelewa kwamba nikitembelea pale atapata mambo mengi na mema. Nimhakikishie tu kwamba tutakwenda pamoja, tutatafuta moja ya *weekend* tukiwa katika kipindi cha Bunge hili refu tufike ili tuone hizo kero ambazo amezitungumza. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nini mpango wa Serikali kuhusu kuongeza vifaa tiba kwenye Kituo cha Afya Nyamwaga, Wilaya ya Tarime ili kipandishwe hadhi kiwe Hospitali ya Wilaya, ikizingatiwa Wilaya ya Tarime ina uhitaji mkubwa kutokana na jioografia ilivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ambacho Mheshimiwa Mbunge ameomba tu hapa ni kwamba, lini Serikali tutaongeza fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Nyamwaga ili kiweze kuendelea kuhudumia watu? Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imesikia ombi lake na tutafanya tathmini tuone ni vitu vingapi ambavyo vinahitajika kwa wakati huu ili viweze kutoa ile huduma stahiki. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aliyetangulia, Mheshimiwa Ummy, alipita Jimbo la Kalenga na akaahidi kunipa shilingi milioni 300 katika Kituo cha Magulirwa pamoja na cha Kibena: Je, ni lini hizo fedha zitakuja ili tuweze kumaliza vituo hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ambacho amekiainisha hapa Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, Mheshimiwa Waziri alienda akatoa *commitment* ya kupeleka fedha. Nasi tuna mpango wetu pale Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwamba ahadi zote za viongozi zipo katika mipango yetu. Kwa hiyo, litakapokuwa

limekamilika hili, basi hizi fedha ambazo zimeahidiwa zitapelekwa katika hayo maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri aliahidi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kuuliza Serikali, Kata ya Vunta katika Jimbo langu la Same Mashariki lina kituo cha afya ambacho kina jengo moja tu. Sasa Serikali naomba niulize kwamba, mnafanya mpango gani wa kurekebisha ili kiwe kituo cha afya hasa chenye majengo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hayo maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anaeleza, mimi mwenyewe nimefika katika Tarafa ya Mamba Vunta kule, ni milimani kweli kweli; na nimeona changamoto ambayo Mheshimiwa Mbunge ameianisha. Nami nikiwa kule niliwaahidi wananchi kupitia maombi ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kutokana na mahitaji na umbali wa eneo lile tutapeleka kituo cha afya katika Tarafa ile nyingine. Kwa hiyo, ile ahadi ambayo nimeizungumza ipo katika bajeti inayokuja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ondoa shaka katika hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Serikali ilijenga Kituo cha Afya

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mtakanini na kumaliza mwaka 2020, lakini mpaka leo hakina vifaatiba hasa katika majengo ya upasuaji: Je, ni lini Serikali itanunua vifaatiba katika Kituo cha Afya cha Mtakanini? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, vile vituo tulivyoanza navyo, kuna vituo vya mwanzo ambavyo tulitoa fedha na ambavyo vimeshakamilika, tumeshaanza kupeleka fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba ili vile vituo vianze kukamilika; na tutapeleka hivyo katika awamu ya pili. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, lipo katika mpango na watapata hivi karibuni. Nimhakikishie kwamba hicho kituo cha afya na chenyewe kinaanza kufanya kazi kwa sababu nafahamu kwamba hii ni *commitment* ya Serikali na fedha ipo na tumekuwa tukifanya hivyo. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa changamoto iliyoko Busega inafanana kabisa na changamoto iliyoko Wilaya ya Kiteto: Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa vituo vya afya katika Tarafa zifuatazo: Tarafa ya Dosidosi, Tarafa ya Makame pamoja na Tarafa ya Kibaya? Ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hapo unataka yote hayo akujibu saa hizi na hilo ni swali la nyongeza?



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, yeye ameomba kwamba, vituo vitatu katika Tarafa tatu ambazo ameziainisha hapo.

Mheshimiwa Spika, unatambua kabisa kwamba Serikali ya Awamu ya Sita, moja ya kazi kubwa ambayo tumeifanya sasa hivi ni kuhakikisha Tarafa zote ambazo hazikuwa na vituo vya afya, tumepeleka fedha na ujenzi unaanza.

Kwa hiyo, miongoni mwa maeneo ambayo ameyataja, zipo baadhi ya Kata, sehemu ya hizi Tarafa alizozitaja, tumepeleka vituo vya afya na ujenzi unaendelea. Kwa hiyo, nimwondoe shaka kwamba hivyo vituo vitakamilika na tutaleta na vifaa tiba ili kuhakikisha wale wananchi wanapata huduma ya afya kama ambavyo Serikali imekusudia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatey Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la Busega ambalo ni la msingi...

**SPIKA:** Ngoja, kabla hujazungumza. Waheshimiwa Wabunge, habari ya kufananisha mazingira tunapoteza muda. Nenda moja kwa moja kwenye hoja yako. Mazingira Waziri anayajua, kwa hiyo, siyo lazima ulinganishe swali la msingi na la kwako, nenda moja kwa moja kwenye la kwako.

Mheshimiwa Flatei Massay.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Halmashauri ya Mbulu Vijijini haina vifaatiba. Je, Serikali ina mpango gani kuleta vifaatiba kwenye Halmashauri hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilijibu kwa Wabunge wa awali kuhusu vifaatiba ni kwamba, sasa hivi moja ya jukumu kubwa ambalo tunalifanya sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ni kupeleka fedha kwenye hospitali na vituo vya afya ambavyo vimekamilika kwa ajili ya kununua vifaatiba; na hilo limekuwa likifanyika. Kwa hiyo, hata yeye katika Halmashauri yake najua kwamba akiwasiliana nao kule kuna fedha nyingine tumepeleka Machi, mwaka huu kuhakikisha wananchi wale wanapata vifaatiba. Kwa hiyo, hilo ndiyo jibu la Serikali kwa ujumla katika maeneo yote ambayo yanahitaji vifaatiba. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi: Kituo cha afya cha Lupa Tingatinga ndiyo kituo cha afya kikubwa zaidi kwenye Tarafa ya Kipembawe, lakini kituo hiki hakina wodi yoyote kwenye Tarafa hii. Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kujenga wodi kwenye Kituo cha Afya cha Lupa Tingatinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika,

ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameanisha hapa kwamba, kwenye Kituo cha Afya cha Lupa Tingatinga, na bahati nzuri hili eneo nalifahamu na changamoto zake nazijua, ninajua kazi ambayo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akipambania pale ni wananchi wake kupata wodi. Nimhakikishie tu kwamba, tutaliweka katika mipango ya Serikali ili tuhakikishe wanapata wodi na hicho kituo kiendeleo kutoa huduma. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Twaha Mpenbenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kibiti kwenye Kata ya Bungu tuna ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kutupa shilingi milioni 250 kumalizia kituo cha afya. Ni lini Serikali italeti fedha hizo ili tuweze kumalizia kile kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Twaha Mpenbenwe, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, tulishatoa fedha awamu ya kwanza shilingi milioni 250 katika vituo ambavyo asilimia kubwa ya Wabunge walipata, ikiwemo katika Jimbo la Kibiti ambalo Mheshimiwa Mbunge ameanisha. Nimhakikishie tu kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha tutatoa fedha nyingine shilingi milioni 250; na katika awamu ya kwanza tayari vituo vya afya 100 tumeshapeleka

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

shilingi milioni 250 kumalizia ile shilingi milioni 500 na bado vituo vya afya kama 123 ambavyo tutamalizia kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha watapata hiyo fedha, shilingi milioni 250 ili waweze kumaliza vyote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Zahanati ya Mabwepande imechakaa na kusababisha wananchi na watumishi kuhudumiwa nje ya kituo chini ya mti: Je, ni lini Serikali itaenda kukarabati zahanati hiyo au kujenga kituo cha afya ili wananchi wa Mabwepande waweze kupata huduma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felister Njau swali huwa ni moja, sasa naona unataka kuunganisha na kiunganishi 'au'. Mheshimiwa Naibu Waziri, wewe jibu swali linalohusu ukarabati wa zahanati.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya mpango ambao sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tulikaa na Halmashauri zenye mapato makubwa ikiwemo Halmashauri ya Kinondoni, Jiji la Dar es Salaam pamoja na Ilala na Temeke. Tuliwaambia kwamba, kwa sababu maeneo yenu yana fedha kubwa, basi mhakikishe mnatenga fedha kwa ajili ya ukarabati. Kwa hiyo, kupitia swali hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amesainisha hapa, nimwagize Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kinondoni kuhakikisha kwamba anapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa kituo cha afya cha Mabwepande. Ahsante sana.

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, ahsante sana kwa majibu yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 4

**Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF)**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuingiza Wananchi wengi zaidi kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unaendelea katika maeneo ya Mamlaka 186 ikiwa ni Halmashauri 184 za Tanzania Bara na Zanzibar. Katika kipindi hiki, idadi ya walengwa iliyobaki awali ya asilimia 30 ya Vijiji, Mitaa pamoja na Shehia 7,217 ambazo hazikufikiwa katika kipindi cha kwanza imeongezwa. Jumla ya kaya 498,091 zilizokidhi vigezo zimeandikishwa na kuingizwa kwenye mifumo ya taarifa za walengwa. Aidha, Kaya mpya na ambazo zilikuwemo kwenye Mpango, zinafanya jumla ya idadi kuu ya walengwa kuongezeka na kufikia kaya 1,279,325.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Waziri kwa majibu yake

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mazuri ambayo yanatia moyo na vile vile niwapongeze Mawaziri wangu hawa wa Utumishi kwa jinsi wanavyofanya kazi, wanafanya kazi sana katika hasa masuala haya ya *TASAF* wanafanya kazi kutoka hapa Tanzania Bara mpaka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nina swali moja tu la nyongeza, pamoja na jitihada hizo Serikali inasema nini katika kuhakikisha wanaofikiwa ni walengwa zaidi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ndejemi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeboresha kwanza mifumo ya namna ya kuweza kuwapata walengwa na tumeenda kidigitali zaidi, wale waandikishaji wanatumia teknolojia, kwa kutumia *tablets* (vishikwambi), kuwaingiza walengwa katika mfumo wa *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna mfumo mwingine ambao umeongezwa wa malalamiko kwa wale ambao wanaona huenda walistahili kuwemo kwenye mpango wa *TASAF*, lakini waliachwa, basi kuna mfumo wa malalamiko na yale malalamiko yao yakiwekwa huwa yanapitiwa na wataalam wa *TASAF* na kuweza kuwarejea kuwahakiki tena na kuona kama wanastahili.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba mfumo uliowekwa wa namna ya kuwapata walengwa wa kaya maskini huwa hauanzii juu kwenda chini, mfumo ule unaanzia chini kwenda juu kwa maana Serikali ya Kijiji na wananchi hukutana katika mikutano ya kijiji na wanaanza kwa kutambuana wao kwamba fulani ni kaya maskini fulani si kaya maskini. Kwa hiyo, mfumo ule umeanza toka kijijini kuja mpaka juu sasa tayari Serikali imechukua hatua hizo lakini tunazidi

kusisitiza wale wanaoenda kuandikisha kule kwa kushirikiana na Watendaji wetu wa Vijiji na Kata kuwa wakweli na kuhakikisha haonewi mtu katika wale wanaostahili kuingia katika mpango wa *TASAF*, basi waingizwe katika mpango wa *TASAF* nao waweze kuwa katika walengwa ambao wananufaika na mradi huu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Ikupa, swali la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri simama tu hapo hapo subiria maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Stella Ikupa, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, kwenye mpango huu wa kunusuru kaya maskini kulikuwa na mapendekezo ya kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu wanaokidhi vigezo. Je, ni kwa kiasi gani mapendekezo hayo yamezingatiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kimewekwa hasa kwa watu wenye mahitaji maalum na kuangalia kwamba wanakidhi vigezo vile. Kwa sababu unakuta kuna watu wana hitaji maalum wenye ulemavu, lakini wanapopitiwa na dodoso lile wanagundulika kwamba vigezo vile vinavyotakiwa kuingia katika kaya ya walengwa hawajavifikia, lakini wengi ambao wamefikia huwa wanapewa kipaumbele na wanaingizwa katika mpango.

Mheshimiwa Spika, nimwongezee tu Mheshimiwa Mbunge, tunayo vile vile program ambayo inasaidia watu wenye ulemavu ili kuwa kwenye vikundi vya uzalishaji na wanapewa fedha kutoka Mfuko huu wa *TASAF* kuweza kuanzisha biashara zao, kwa hiyo tunatoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru lengo la mfuko huu ni kusaidia kaya maskini lakini unakuta bado haileti tija kutokana na pesa ambazo wanatoa elfu 50, laki, mwisho tunawafanya wanakuwa tegemezi. Ni mkakati gani wa Serikali kuhakikisha unabadilisha huu mfumo na matokeo yake kwenda kuwapa mitaji ili wasiendelee tena kutegemea zile 50, 50 waweze kukidhi maisha yao moja kwa moja? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, tunatoa elimu kwa wale waratibu wetu kule chini na wao waweze kutoa elimu kwa walengwa ya namna bora ya kuweza kuzitumia fedha hizi wanazozipokea. Tukiangalia kwamba kaya hizi nyingi zilikuwa hazina uhakika wa kula yao, hazina uhakika wa milo mitatu.

Kwa hiyo kwa kuingia kwenye mpango huu kwa kupata kiwango cha fedha ambacho Mheshimiwa Bulaya amekitaja na wengine hupata zaidi, imeshawapa *boost* ya kutosha ya kuweza kuanza kufuga kuku, mbuzi ili kuweza kuboresha maisha yao na kuwa na uhakika wa kula kila siku.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunawasisitiza sana wenzetu wa Serikali za Mitaa kwa maana Wakurugenzi kule kuhakikisha wanawaweka hawa walengwa katika mpango wa ile 4, 4, 2. Kwa sababu kwenye kaya hizi maskini wapo akinamama, kwenye kaya hizi maskini wapo walemavu, kwenye kaya hizi maskini wapo vijana. Kwa hiyo tunasisitiza sana kwamba hawa walengwa waliokuwepo kwenye kaya hizi kuweza kuingia katika 4:4:2 ili waweze kupata mkopo wa vikundi kuweza kuongeza kipato na kuweza kufanyabiashara mbalimbali.



**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa mpango huu kwa Wilaya ya Rorya kuna vijiji zaidi ya 20 na nimeshamtumia Mheshimiwa Waziri, ambavyo wengi wao wame-*raise* malalamiko ya kuachwa kwenye mpango wenyewe kipindi unatekelezwa. Nataka nijue nini mkakati wa Wizara kwenye vile vijiji ambavyo hasa watu wanalalamika kwamba waliachwa kipindi cha awali katika mpango wa utekelezaji wa *TASAF*. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, naomba nimjibu Mheshimiwa Chege kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jibu ni hivyo hivyo kwamba kaya zote ambazo zilikuwa zimeachwa na zinastahili kuingia katika mpango, awamu hii ya pili zinaingizwa zote kwenye mpango huu. Vile vile vijiji vyote ambavyo vilikuwa vimesalia havikuingia kwenye mpango huu wa *TASAF*, sasa vinaenda kuingia katika mpango huu wa *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, sasa huenda nione ni namna gani nitakutana na Mheshimiwa Chege ili tuweze kupanga, tuone tunasaidiaje hivi vijiji 20 ambavyo anavyo jimboni kwake, kuweza kuona tunakwenda kuziona ama tunawaelekeza wenzetu wa *TASAF* waweze kufika katika jimbo la Mheshimiwa na kuona tunawasaidiaje walengwa hawa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 5

## **Hitaji la Miradi ya Umwagiliaji Tarafa ya Malangali**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga miradi ya umwagiliaji katika Tarafa ya Malangali ili wananchi waweze kushiriki katika kilimo cha umwagiliaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Mwkiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Iringa unakadiriwa kuwa na eneo linalofaa kwa kilimo la hekta 54,000. Kati ya hizo hekta 20,017 zinamwagiliwa ambapo hekta 16,789 zinamwagiliwa kipindi cha masika na hekta 3,550 zinamwagiliwa kipindi cha kiangazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na uhakiki wa maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya ya Mufindi ambapo hadi sasa skimu nne (4) zenye jumla ya hekta 1,800 zimehakikiwa na kuwekwa kwenye mpango wa umwagiliaji. Aidha, Tume inaendelea na uhakiki wa maeneo mengine yanayofaa kwa umwagiliaji ikiwemo Tarafa ya Malangali.

Mheshimiwa Spika, zoezi la uhakiki litakapokamilika, Tume ya Umwagiliaji itaandaa mpango kazi utakaoainisha kazi zitakazofanyika katika skimu hizo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Mwkiposa Kihenzile swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tarafa ya Malangali hususan Kata za Nyololo, Maduma, Ihoanza, Idunda mpaka Mbalamaziwa wanafuatilia kwa umakini sana pengine kufahamu *commitment* ya Serikali, ni lini sasa kwa maana kama ni mwezi au kama ni mwaka wa fedha watapata matumaini ya kupata huu mradi wa umwagiliaji kutokana na changamoto kubwa sana ya ukame kwenye maeneo yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji na Serikali pia inatambua kwamba eneo la Mufindi ni kati ya maeneo ambayo kuna wakulima wengi na uzalishaji wake utaoongeza tija kwenye kilimo cha nchi yetu ya Tanzania. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti inayokuja kwa maana kuanzia mwezi Julai tutatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uhakiki huo unakamilika, tukisha-*establish* mahitaji baada ya hapo sasa tutakwenda kwenye hatua inayofuata ambayo itakuwa ni hatua ya ujenzi kutokana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge na kwamba zoezi hilo litaanza mapema mwezi wa Saba ambapo uhakiki huu utafanyika na baadaye tutaenda katika hatua ya ku-*establish* mahitaji.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Bwawa la umwagiliaji la Edayaya Tlawi katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu ilifanyiwa usanifu toka 2009; je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo?

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mikakati ambayo tumeiweka hivi sasa kama Wizara, tumeiagiza Tume ya Umwagiliaji wa Taifa ku-*take stock* ya miradi yote ya umwagiliaji katika nchi yetu ya Tanzania ile ambayo ilishafanyiwa upembuzi yakinifu ambayo ilishafanyiwa usanifu na baadaye kinachofanyika ni kwamba tutakwenda katika mradi mmoja baada ya mwingine iko miradi ambayo inahitaji fedha kidogo na iko miradi ambayo inahitaji fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, kupitia maelekezo haya ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa, Tume hivi sasa wameanza zoezi hilo. Tutaipitia miradi yote na hivi sasa tunayo miradi 51 ambayo imeshatangazwa kupatikana kwa wakandarasi, naamini kupitia utaratibu huu ambao tumeuanzisha, tutaifikia miradi yote ikiwemo mradi ambao Mheshimiwa Mbunge ameusema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika Manispaa ya Iringa katika Kata ya Isakalilo kuna Mradi wa Mkoga katika Kata ya Kituli kuna Mradi wa Kitwilu. Hii miradi ni ya muda mrefu sana. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kutoa pesa ili wananchi hasa akinamama na vijana waweze kujiajiri kupitia hii miradi kwa kulima mbogamboga na matunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya awali kwamba miradi yote hii na hasa katika Mkoa wa Iringa tumeshatenga fedha tayari kwa ajili ya Tume yetu kukamilisha kazi hii ya uhakiki. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais ametuongezea bajeti kutoka shilingi bilioni 17 mpaka bilioni 51, nataka nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba katika kuelekea ajenda 1030 ya kukuza kilimo katika nchi yetu, moja ya kipaumbele ni kilimo cha umwagiliaji, hivyo hatutaacha mradi wowote nyuma, miradi yote tutajenga tukipata fedha ambazo zitatuwezesha kufikia malengo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri; je, mifereji iliyo kwenye Kata ya Kilema na Kirua Vunjo na ile skimu ya Kahe wanaifahamu? Mbona haijawahi kuangaliwa siku za karibuni? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi yote ya umwagiliaji nchini inafahamika na ndiyo maana katika maelezo yangu ya awali nilisema tunayo miradi mingi sana. Tumeielekeza Tume badala ya kuendelea kukumbatia miradi mingi ambayo haifanyi kazi, tunaanza ku-*take stock* kupata mradi ambao unahitaji marekebisho madogo, mradi ambao unahitaji marekebisho makubwa, baadaye tuweke nguvu kukamilisha miradi hii ikiwemo mradi wa Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Amar swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kuna

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

bwawa kubwa pale Kijiji cha Nyamgogwa, Kata ya Shabaka tumeshafanya upembuzi yakinifu na tumeshapeleka andiko mezani kwa Mheshimiwa Waziri, tunahitaji milioni 500 kwa ajili ya kulifufua ama kuliandaa bwawa hilo ambalo linanufaisha zaidi ya vijiji 20. Je, Waziri anatoa majibu gani kuhusu andiko letu hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Amar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge andiko lake kweli lipo mezani na hivi sasa kwa sababu ya ufinyu wa bajeti tumekuja na mfumo mwingine ambao pia umesaidia ujenzi wa skimu hizi ambao tunakwenda kuutambulisha mfumo huu. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba na yeye pia tutamuingiza kwenye mfumo huo ambao tumeufanya na tumeanza kuufanya kwa Mheshimiwa Mtaturu pale katika miradi ya Magonyi.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu tutamchukua benki, tutamchukua na *off taker* wa mazao ya wakulima na kwa pamoja tunamwomba benki arekebisha miundombinu ya eneo lile, halafu mazao yatakayolimwa katika eneo lile tutamtafuta muuzaji ili basi itumike gharama hiyo ya benki kurekebisha. Wakati huo huo wauzaji wapate uhakika wa mazao yao ya kilimo na mwisho wa siku tutakuwa tumetatua changamoto ya ukosefu wa masoko ya wakulima wetu, lakini pia mradi huu utakuwa umekamilika. Mfumo huu unaitwa *Tripartite Agreement* ndiyo ambao tunaenda kuutekeleza katika miradi mingi ya skimu za umwagiliaji. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la

nyongeza. Kwa sababu miradi mingi ambayo Serikali inaiongelea ni ile ambayo ilijengwa miaka ya zamani na teknolojia ambayo imekuwa ikitumika ni ile ambayo ni ya mifereji ambayo inatumia maji mengi sana na inaharibu maji *unnecessary*. Kuna teknolojia mpya ambayo inatumika na tunaona katika nchi za jirani. Je, Serikali iko tayari kwenda kutumia teknolojia mpya ambayo inatumia maji kidogo lakini inakuwa na ufanisi zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Serikali tupo tayari kuendelea kutumia teknolojia ambayo italeta ufanisi katika kilimo cha umwagiliaji na hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri na mimi mnatuona pale ni vijana ambao pia ni wa kidigitali, kwa hiyo tutahakikisha ya kwamba tunapitia kuona mifumo mbalimbali hasa yenye kuleta ufanisi ambayo naamini kabisa kama ni mfumo ambao Mheshimiwa Mbunge amezungumza hapa ambao utaleta tija kwa wakulima wetu sisi tuko tayari kuutumia mfumo huu na tutaelekeza pia Tume ya Umwagiliaji kuhakikisha kwamba inafanya utafiti wa kugundua teknolojia mbalimbali ili kumletea tija mkulima wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka swali la Nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Tarafa ya Gonja katika Wilaya ya Same kwa takriban miaka kumi sasa wameomba kujengewa Bwawa la Yongoma ili lisaidie umwagiliaji katika Kata kame za Ndungu na Maore na *design* ilishafanywa na wajapan tangu 2012. Je, ni lini Serikali itajenga bwawa hili? *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaboyoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti inayokuja mwaka 2022/2023 tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa 19, natumai pia na bwawa la Mheshimiwa litakuwemo ndani ya ujenzi huo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum...

Samahani Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako, ahsante sana.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 6

### Uhitaji wa Magari Mapya ya Polisi Nchini

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua magari ya Polisi kwa ajili ya vituo vya Polisi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engineer* Masauni, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu na uhitaji wa kulipatia Jeshi la Polisi magari kama nyenzo za kutendea kazi. Kupitia mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya *Ashok Leyland* ya nchini India, Serikali inategemea kupokea magari 369 kutoka nchini India ifikapo Septemba, 2022 ambapo mwishoni mwa mwezi Aprili, 2022 tunatarajia kupokea magari 78 yameshakaguliwa na kuthibitishwa. Magari hayo yatakapofika yatagawiwa kwenye Vituo vya Polisi vyenye uhitaji mkubwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nimshukuru Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa, nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Kilimanjaro ni mojawapo ya Mikoa ambayo ina uhitaji wa magari ya polisi hasa magari ya doria; je, Serikali ina mpango gani Mkoa wa Kilimanjaro kupata magari katika awamu hii ya kwanza ya magari 78 ambayo yanaingia nchini mwezi Aprili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kutokana na jitihada zake anazochukua za kuhangaikia Mkoa wake wa Kilimanjaro basi tumepokea mapendekezo yake na tutahakikisha kwamba magari haya yakija tutaangalia uwezekano vilevile tuweze kupeleka Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri usiondoke subiri maswali ya nyongeza, eeh hapo hapo ili tupunguze muda wa kutembea.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Juliana Shonza swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Mkoa wa Songwe ni mpya na upo mpakani na kwenye jibu la Mheshimiwa Waziri amesema kwamba magari yatapeleka kwenye maeneo ambayo yanahitaji mkubwa, Mkoa wa Songwe una uhitaji mkubwa wa magari ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu nini ahadi ya Serikali katika kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ya magari katika Mkoa wa Songwe? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi kwamba magari yale yatakapokuja tutayapeleka katika Mikoa ambayo ina uhitaji zaidi na Mheshimiwa Mbunge amethibitisha kwamba Mkoa wa Songwe ni moja kati ya Mikoa ambayo ina mahitaji basi tatalizingatia hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba hali ni mbaya katika Wilaya ya Mbozi hivi ninavyoongea Mkuu wa Polisi wa Wilaya hana gari hata la kutembelea. Kwa hiyo, katika hayo magari 78 Mheshimiwa Waziri naomba

unihakikishie gari moja liende katika Wilaya ya Mbozi ili kumuokoa yule Mkuu wa Polisi wa Wilaya. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nitakuwa sijakosea nadhani Wilaya yake ndiyo ile ya Mheshimiwa Silinde, kama hivi ndivyo hivi karibuni tulipeleka gari huko ambalo halikuwa jipya, kwa hiyo litasaidia nadhani tatizo litakuwa limepata ufumbuzi kama itakuwa siyo Wilaya hiyo ni Wilaya nyingine basi tutalizingatia vilevile. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Naona Waheshimiwa Wabunge wamesimama wengi lakini sasa mmeshaambiwa awamu ya kwanza ni magari 78 tu sasa sijui litaenda wapi liache wapi, Mheshimiwa Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale ilikuwa na gari moja tu ambalo kwenye Uchaguzi uliopita gari lile lilichomwa moto mpaka sasa hivi Wilaya nzima ile haina gari hata moja. Ni nini mpango wa Serikali kutupatia miongoni mwa hayo magari 78?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba maswali yetu yasimuweke mazingira ambayo Mheshimiwa Waziri anatakiwa kuwa na ile orodha ya magari yale 78 yanaenda wapi, wewe uliza tu uhitaji wa Jimbo lako maana sitaki sasa kumuweka hapa akawa anaahidi kila Mbunge halafu magari yako 78 Wabunge tupo 393 humu ndani. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kuliweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu sasa swali la Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi kwamba magari haya yatakapokuja tutayapeleka katika maeneo ambayo yana mahitaji zaidi, kwa kweli maeneo ambayo yana mahitaji zaidi ni mengi kwa hiyo siyo rahisi kuweza kukamilisha kwa wakati mmoja kwa mwezi huu.

Kwa hiyo, niombe nikubaliane na Mheshimiwa Spika kwamba hoja za Waheshimiwa Wabunge tunajua ni za msingi, lakini magari yatakuja kwa awamu basi tutazingatia wapi kuna mahitaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika maswali yaliyopita ikiwemo na Mheshimiwa Mbunge Kuchauka kama itaangukia katika maeneo ambayo yana mahitaji zaidi na zaidi utapata mapema lakini nikuhakikishe kwamba tunafahamu na tunafanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dorothy Kilave swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana swali langu dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na magari mengi ambayo mmeyatuma yatakuja kwa awamu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutenga fedha za kutengeneza magari yaliyopo ambayo ni mengi tunayaona yapo katika vituo vingi vya Polisi ni mabovu. Sasa ni wakati mzuri labda muweze kutenga fedha ili tuweze kutengeneza haya yaliyopo tukisubiri hayo mageni, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilave Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja yake ni ya msingi lakini nimhakikishie kwamba tumekuwa tukifanya hivyo na hata ndani ya Jeshi la Polisi tuna kitengo maalum kwa ajili ya matengenezo ya magari ya Polisi yale ambayo yanaweza kutengenezeka tunafanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tunafikiria kuja na mpango mwingine ambao utasaidia sana kuweza kutatua changamoto ya ubovu wa magari, nadhani wakati tutakapokuja kuwasilisha bajeti yetu hapa tutakuwa na nafasi pana zaidi ya kuweza kufafanua, lakini nimpongeze kwa wazo lake ni zuri na tunaendelea kulifanyia kazi na tutazidi kuliboresha zaidi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mwangao Tabasam swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri ni kwamba hali ya gari la Sengerema anajua mpaka Mheshimiwa Simbachawene aliniahidi mwaka jana tutapata gari jipya. Sasa haya magari yanayokuja mwezi huu unanihakikishia gari moja linakwenda Sengerema kwa sababu hali iliyopo ni mbaya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hilo nimekupa mwongozo wa jumla, kwa hiyo na wewe jibu kwa jumla.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tabasam Mbunge wa Sengerema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama mwongozo wako ulivyotoa na kama ambavyo nimejibu nyuma kwamba tutapeleka magari haya kulingana na uhitaji zaidi, kwa hiyo tutaangalia kama Jimbo la Sengerema limeangukia katika eneo hilo

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

atapata kama itabidi asubiri basi atapata siku za mbele pale ambapo yatapatikana magari ya ziada.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zidadu Kungu swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tunduru ni Wilaya ambayo ipo mpakani na jioografia yake ni mbaya lakini pia kituo cha polisi kuna gari moja tu na tuna kilomita za mraba 18,778.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kunihakikishia kwamba katika magari hayo 78 nasi tutapata gari moja? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee tena majibu yangu kama ambavyo nimejibu mwanzo kwamba tunatambua kwamba Jimbo la Tunduru lina uhitaji wa gari basi na lenyewe vilevile tumepokea.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa tuendelee na swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini.

Na. 7

**Ukosefu wa Vituo vya Polisi Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Polisi katika Tarafa za Kipatimu, Njinjo na Nanjilinj Wilayani Kilwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga vituo vya Polisi katika maeneo mbalimbali nchini ili kuhudumia wananchi katika kudhibiti uhalifu. Katika Tarafa ya Nanjilinj kinajengwa kituo cha Polisi kitakachogharimu shilingi 67,700,000. Kituo hiki kiko kwenye hatua ya umaliziaji ambapo jumla ya shilingi 62,000,000 zimetumika. Wizara kupitia Jeshi la Polisi itatenga kiasi cha shilingi 5,700,000 ili kukamilisha ujenzi huo kama njia ya kuunga mkono juhudi za wananchi waliochangia ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauri wananchi wa Tarafa za Kipatimu na Njinjo kutenga maeneo ya kujenga vituo vya polisi na kuanza ujenzi na Serikali itaunga mkono kama ilivyofanya katika Tarafa ya Nanjilinj.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, nina maswali mawili;

Kwanza, kwa kuwa katika Tarafa mbili zilizobaki ambazo Serikali bado hajjawekeza ujenzi wa vituo vya Polisi, kumekuwa na changamoto kubwa ya mapigano kati ya wafugaji na wakulima lakini wakati huo huo Tarafa hizo zipo

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

umbali mrefu sana kutoka kule ambapo vituo vya Polisi vipo hivi sasa;

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu katika Tarafa za namna hii zenye changamoto kubwa ya wakulima na wafugaji kuweza kuwekeza kama ilivyowekeza katika sekta nyingine ujenzi wa Vituo vya Afya kwa kuanzia na bajeti ya mwaka huu? *(Makofi)*

Pili, ningeomba Mheshimiwa Waziri anifahamishe ni lini atakuwa na nafasi ya kuweza kutembelea katika Wilaya ya Kilwa ili tuweze kushirikiana na Wizara yake katika kutatua changamoto ambazo zinakabili upatikanaji wa vituo vya Polisi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Francis Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza alitaka kujua mpango wa Serikali wa kujenga vituo vya Polisi kama vile ambavyo tunafanya katika vituo vya Afya na shule, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba wazo lake tumeshaanza kulifanyia kazi, tulikuwa na mazungumzo kati ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Wizara ya TAMISEMI.

Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa kulipokea wazo hili na hivi sasa tunavyozungumza wataalam wetu, Makatibu Wakuu wa Wizara hizi mbili na wataalam wetu wanakaa kuangalia uwezekano huo kupitia kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili ni jambo ambalo tunalichakata na kama litakuwa limekwenda vizuri tunaweza



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tukaliwasilisha hapa Bungeni kulingana na mapendekezo ambayo wataalam watatupatia.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la mimi kutembelea, hilo halina mjadala. Nimhakikishie Mheshimiwa Francis Ndulane kwamba tutapanga ratiba ili tuweze kwenda katika Jimbo lake kuhamasisha wananchi, kama vile nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba kama wananchi wataweza kufanya utaratibu wa kupata eneo na hata wakianza wa kwa nguvu zao, kama ambavyo kuna maeneo Waheshimiwa Wabunge wamefanya, naye pia alifanya hivyo katika baadhi ya vituo vyake, hata juzi hapa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula katika Jimbo lake pale, alifanya jitihada za kuhamasisha wananchi kujenga Kituo cha Polisi Ilemela. Kwa hiyo, jitihada kama hizi tutaziunga mkono.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ndulane ninajua jitihada zake katika kupigania wananchi wake na hivyo basi nimhakikishie tutashirikiana kutafuta njia mbadala ya haraka wakati tukisubiri mipango ya muda wa kati na muda mrefu wa Serikali kutatua changamoto hii kwa kudumu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Ungele swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi Mkoa wa Lindi yana changamoto ya usalama hasa katika migogoro ya wakulima na wafugaji hata wakati wa msimu wa korosho na ufuta usalama wa wananchi unakuwa mgumu. Maeneo mengi yapo mbali na Makao Makuu ya Wilaya, mfano Kilimarondo ipo kilometa 120, Nambiranje Wilaya ya Ruangwa napo ni mbali, pia Nangaru Wilaya ya Lindi.

Je, Serikali itajenga lini Vituo vya Polisi maeneo hayo ili kuwahakikisha usalama wa wananchi. Ahsante?  
(Makofi)

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na changamoto hiyo ama uhitaji huo wa vituo vya Polisi katika Mkoa wa Lindi, lakini kuna kazi ambayo tayari tumeshaanza kuifanya. Kwa mfano, katika bajeti hii ambayo tunaendelea nayo kuna maeneo ambayo Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo vya Polisi na hata bajeti inayokuja tumezingatia hilo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hatuwezi kutatua changamoto hii kwa wakati mmoja kwa maeneo yote, lakini nitakapokuja kwenye ziara kuitembelea Kilwa Kaskazini nitamuomba Mheshimiwa Mbunge nae tuwe pamoja ili tuangalie namna gani tunaweza kuharakisha utatuzi wa changamoto hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naamini Serikali inafanya kazi kubwa katika sekta zote, ninaamini na kujua kwamba ulinzi na usalama ni jambo muhimu sana katika ustawi wa wananchi na raia wake.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Mchinga lina Kata 11 na Tarafa nne, Tarafa mbili tu ndiyo zenye Vituo vya Polisi. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba Tarafa hizi Mbili zilizobaki zinapata Vituo vya Polisi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salma Kikwete Mbunge wa Mchinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nijibu kwa ujumla wake kwamba mahitaji ya vituo vya Polisi kwa kweli ni makubwa labda nitoe mfano mmoja tu. Vituo Daraja 'B' vilivyopo ni 93 wakati mahitaji ni 563 utaona tofauti ilivyokuwa pana sana, kwa hiyo changamoto hii ipo maeneo mengi ikiwemo kwenye Jimbo la Mheshimiwa Salma Kikwete Mchinga.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba kama Serikali tunatambua changamoto hiyo na tupo katika hatua ambazo nyingine nilizieleza katika majibu yangu ya awali na hivyo basi tupewe muda ili tuweze kutatua changamoto hii kwa mapana yake kwa ujumla katika maeneo yote ambayo yana changamoto ikiwemo Jimbo la Mchinga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Monni swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Chemba ujenzi wake umesimama kwa miaka minne sasa, naomba kumuuliza Waziri ni lini sasa watatoa fedha za kumalizia? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa kumaliza vituo vya Polisi tumekuwa tukitumia njia mbalimbali ikiwemo kutumia Mfuko wetu wa Tuzo na Tozo ambao upo chini ya Jeshi la Polisi, ambao katika mwaka huu wa fedha tumeshaufanyia ujenzi na ukarabati wa vituo kadhaa katika maeneo mbalimbali nchini. Hivyo basi nichukua hoja hii ya kituo cha Chemba tuona kama tunaweza kumaliza kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo katika kipindi cha mwaka huu wa fedha unaokuja.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, tuangalie kimefikia kiwango gani na mahitaji ni kiasi gani na uwezo wa fedha zilizopo ni kiasi gani na vipaumbele vilivyopo ni vipi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Katavi na Wilaya zake kumekuwa na wimbi la mauaji ya mara kwa mara hii ni kwa sababu hakuna vituo vingi vya polisi.

Je, ni lini mtatujengea kituo cha Polisi katika Kata ya Kasekese Wilaya ya Tanganyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Kakoso kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninaomba nilichukue hili tulifanyie kazi ili tuone hatua ya kuchukua.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaelekea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula Mbunge wa Nyamagana sasa aulize swali lake.

Na. 8

**Ujenzi wa Barabara Kuu ya Mwanza – Shinyanga**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kuu ya Mwanza - Shinyanga kwa kiwango cha njia nne kutoka Mwanza Mjini hadi Usagara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Eng. Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi kwa ajili ya ukarabati wa barabara kuu ya Mwanza, Shinyanga, yenye urefu wa kilometa 104 ambao utahusisha na upanuzi wa barabara kutoka njia mbili kuwa njia nne kwa sehemu ya kutoka Mwanza Mjini hadi Usagara, kilometa 25. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa barabara hii iko katika hatua za mwisho na inatarajiwa kukamilika tarehe 27 Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya usanifu wa kina kukamilika na gharama za ukarabati kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ukarabati utakaohusisha upanuzi wa sehemu ya kutoka Mwanza Mjini hadi Usagara, kilometa 25 kutoka njia mbili kuwa njia nne. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, kwani barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Nyamagana na Jiji la Mwanza kwa ujumla, ukizingatia kwa sasa tuna mradi mkubwa wa daraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na upembuzi yakinifu unaokamilika mwezi huu, naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba baada ya upembezi yakinifu

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kukamilika na bajeti itakuwa imeshaanza, kwenye mapitio ya bajeti, Serikali itakuwa tayari kuhakikisha barabara hii inaingia kwenye mpango na kuanza kujengwa upya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwezi huu wa Nne tarehe 27 tutakamilisha usanifu wa kina. Kama alivyoomba kwamba baada ya kukamilika Serikali itafanya nini kwenye *mid review* ya bajeti ya Wizara?

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imesikia ombi lake, nasi tunajua msongamano wa barabara hiyo. Tumelichukua na tutaangalia jinsi ya kufanya pale itakapokamilika na kujua gharama ya barabara hii. Ahsante. (*Makoff*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. barabara Kolandoto - Munze - Mwangungo yenye kilometa 63 ni barabara ambayo imo katika mpango wa Ilani ya Utekelezaji ya Chama cha Mapinduzi na pia ipo katika mpango wa bajeti ya 2021/2022: Ni lini utekelezaji wa mradi huu utaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara Kolandoto - Mwangungo kwenda Lalago ni barabara ambayo iko kwenye ilani na imekuwa ikipangiwa bajeti. Barabara hii ni ndefu inayokwenda mpaka Sibiti - Mbulu, kwa maana ya Hyadom – Mbulu. Barabara hii imeanza kutekelezwa kwa vipande na kwa sasa tutaanza ujenzi wa kipande cha Mbulu – Hyadom kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2020, wakati anafunga kampeni za uchaguzi katika Jimbo la Ushetu, alipokea simu kutoka kwa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. Magufuli na akawaahidi maelefu ya wananchi pale kwamba atawajengea kilometa 54 za lami kutoka Kahama – Nyandekwa - Iboja mpaka lyogo kilometa 54 za lami: je, ahadi hii itaanza kutekelezwa lini kwa wananchi wa Ushetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumekuwa tukisema, ahadi zote za viongozi wa Kitaifa ni ahadi ambazo zinatekelezwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara zote ambazo zimeahidiwa tunazo lakini tunaendelea kuzitekeleza kadri ya upatikanaji wa fedha ikiwa ni pamoja na hii barabara ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii pia itajengwa kwa kiwango cha lami kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliagiza. Ahsante. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ipo dhamira ya Serikali ya kuunganisha mikoa yote kwa barabara za lami. Mkoa wa Singida ni miongoni ni mwa mikoa ambayo haijaunganishwa na mikoa mingine ukiwemo Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Mbeya.

Je, dhamira ya Serikali ya kujenga barabara ya Mkiwa – Itigi – Rungwa hadi Makongorosi imefikia wapi kuanza kujengwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Massare, Mbunge wa Itigi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni barabara kuu ambayo inatoka Mkiwa – Itigi - Rungwa hadi Makongorosi – Chunya. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ni kati ya barabara 22 ambazo ziko kwenye maandalizi ya kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Mkiwa kwenda Manyoni mwaka huu wa fedha kilometa 50. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara ya kutoka Newala kuelekea Masasi kupitia Mitesa imechukua muda mrefu sana kuanza licha ya kwamba fedha ipo, kwa nini barabara hii imechukua muda mrefu kiasi hiki? Lini barabara hii itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Moja tu Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.



**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nimemsikia vizuri, anaongelea barabara ya Newala kwenda Masasi kuanzia Munivata. Barabara hii ilishapatiwa fedha na ipo kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami. Kwa hiyo, suala tu ni kwamba, mikataba tayari inaandaliwa kwa ajili ya kuanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kuanzia Mnivata, Newala hadi Masasi yenye urefu wa kilometa 160 kama nimemwelewa vizuri

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nami napenda kujua ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha njia nne barabara kuu ya TANZAM, kipande cha Uyole mpaka Songwe kupitia Mbeya Jiji na Mbalizi? *(Makoff)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa swali hilo muhimu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jiji la Mbeya ni kati ya majiji ambayo yana changamoto kubwa sana ya usafiri katika kipindi hiki; na Serikali ina njia mbili ya kutatua changamoto hizi. Moja, ni kujenga *bypass* ya kuanzia Uyole hadi Songwe yenye urefu wa kilomita 49; na pia kupanua barabara inayopita katikati kutoka njia mbili kwenda njia nne.

Mheshimiwa Spika, hatua ya haraka ambayo Serikali imechukua ni kupanua kwanza njia mbili kwenda njia nne kuanzia Uyole hadi Songwe eneo la Ifisi kilomita 29 na taratibu

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

za manunuzi zinaendelea hadi tunavyoongea hapa sasa kwa mwaka huu wa fedha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali lanyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa kuwa barabara kuu ya Makambako – Songea inayopitia katika Mji wa Njombe imezidiwa na inahitaji ukarabati mkubwa: Je, ni lini barabara hii sasa itaanza kukarabatiwa au kujengwa upya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara aliyoitaja ambayo inaanza Makambako, Njombe hadi Songea ni kati ya barabara za zamani sana kujengwa miaka ya 1984. Tayari usanifu ulishakamilika na Serikali inaongea na *Word Bank* ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya kukarabati barabara hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari ipo kwenye mchakato wa kuongea na hizi taasisi za kibenki kwa maana ya kifedha ili tukishafanikiwa basi ukarabati wa barabara hii uanze.

**SPIKA:** Mheshimiwa Phillip Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ujenzi wa barabara ya lami kutoka Mbalizi mpaka Mkwajuni, upembuzi yakinifu na usanifu umekamilika na mwaka huu wa fedha Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, aliniahidi kwamba mwaka 2022/2023 watatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha barabara hiyo lami. Je, anakumbuka; na kwamba tayari mwaka huu wameshatenga fedha za barabara hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mulugo, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ni dhamira ya Serikali kujenga barabara zote kwa kiwango cha lami na hasa zile zinazounganisha mikoa na mikoa, wilaya na wilaya lakini pia barabara kuu na barabara muhimu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali bado iko pale pale. Isipokuwa barabara ipi inaanza, inategemea kimsingi na bajeti ama na fedha itakayokuwa imepatikana kuanza ujenzi.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, dhamira Serikali bado iko pale pale kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na barabara ya Mheshimiwa Mulugo ambayo ameisema. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya *Airport* – Banana, Gongolamboto – Pugu - Chanika ndiyo barabara pekee kwenye Mkoa wa Dar es Salaam ambayo siyo *double road*. Naomba kujua mpango wa Serikali wa kuipanua barabara hii na kuwa ya njia nne.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya kuazia *Airport* kwenda Gongolamboto ni sehemu ya barabara ya *Nyerere Road*. Barabara hii kama nimemwelewa Mheshimiwa Mbunge, ni barabara ambayo ipo kwenye awamu ya tatu ya hizi barabara za kwenda kwa kasi kwa maana ya *BRT*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkataba umeshasainiwa tarehe 17 Machi na Mkandarasi atakayejenga pale ni *Sinohydro*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunategemea muda wowote kuanzia pale katikati ya mji kwenda Gongolamboto barabara hii itaanza kujengwa kwa maana ya kupunguza msongamano kwa wananchi wa Dar es Salaam, hasa kwenye Jimbo la Mheshimiwa Silaa, Ukonga. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilitenga shilingi trilioni 1.5 kwenye Wizara ya Ujenzi na Bunge likapitisha. Mpaka Machi, mwaka huu 2022, imepewa asilimia 68 ambayo ni shilingi trilioni 1.09, hakuna barabara mpya hata moja iliyojengwa katika kipindi hiki cha mwaka fedha, sana sana wamelipa madeni:-

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Serikali, kwanini msiwe wakweli kwa Wabunge hawa, mkawaeleza kwamba mwaka huu tunalipa madeni, na mwaka ujao tunajenga barabara, kuliko kuwapa majibu mazuri ya matumaini wakati fedha hazipo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Waziri wa Fedha amesimama kwa sababu fedha zimezungumzwa hapo. Kwa hiyo, ngoja ajibu yeye. Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu

mazuri aliyoyatoa; na niwahakikishie Wabunge pamoja na Watanzania kwamba fedha za kutekeleza hii miradi zipo; na Serikali inajenga barabara mpya na inalipa madeni. Ujenzi ule unavyofanyika, utaratibu wake ni kwamba kazi inapokamilika ndipo mtu analipwa. Tunalipa kwa *certificate*, hatugawi tu fedha zikasubiri mtu aanze kazi. (Makofi)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kinachofanyika, tunatekeleza mradi, ukishakamilika tunalipa; na tunaendelea na miradi mipya, na yenyewe kadri *certificate* zinavyokuja tunalipa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hiyo anayosema ya madeni inawezekana kwenye hatua nyingine madeni yakawepo, kwa sababu ni lazima tufanye uhakiki; na miradi mingine ilishafanyika katika vipindi tofauti tofauti, kwa hiyo tuna uhakiki na tunalipa.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kweli kwamba tungeweza kujenga reli inayokwenda mpaka *Pacific*, inayokwenda mpaka Bara lingine, inayokwenda mpaka upande mwingine wa bahari, halafu tushindwe kujenga barabara? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote, tunajenga barabara mpya, tunalipa kwa *certificate* zinapokuwa tayari, lakini pia tunalipa na madeni ambayo kazi hizo zilishafanyika.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, hatuwezi tukaacha kutengeneza barabara mpya wala kutekeleza miradi mipya tukafanya kazi moja ya kulipa madeni. Tunalipa madeni na tutatekeleza miradi mipya ya maendeleo.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais na hii ndiyo dira ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, kulikuwa na maswali hayajakamilika, naomba urejee hapo kidogo kwa kifupi tu. Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya Tegeta – Bagamoyo imejengwa na *TANROADS* na kuna sehemu ambayo hawajaweka mitaro kabisa, inasababisha mafuriko katika maeneo ya Basihaya na Tegeta:-

Mheshimiwa Spika, ni nini tamko la Wizara juu ya ku-*repair* eneo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala aliloliongelea la kusababisha mafuriko kwa sababu ya ujenzi wake kwa sababu ya barabara zimeinuka, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumelichukua na ninaomba kutumia nafasi hii nimwagize Meneja wa Barabara wa Dar es Salaam aende akafanye *study* ya nini Wizara tufanye ili tuweze kuondoa changamoto hii kwa wananchi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini sasa Serikali itanza ujenzi wa kiwango cha lami barabara inayotoka Kahama - Geita? Naomba Mheshimiwa Naibu

Waziri anipe majibu ya kweli, barabara hii imekuwa ni kero ya muda mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kahama – Ilogi kwenda Geita ni barabara ambayo inaganisha mikoa miwili; Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Geita kupitia kwenye Jimbo la Mheshimiwa Iddi ambao ni Jimbo la Msalala.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii ni barabara ya kiuchumi na Serikali tumefanya majadiliano na wenzetu wa *Barrick*, lakini imeonekana bado wanasitasita kuanza kujenga hii barabara.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii sasa Serikali itaichukua ili ione namna ya kuifanya na pengine katika bajeti tunayoendelea kuiendea pengine tutaona nini cha kufanya ili tuanze kujenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii niulize swali la nyongeza. Barabara ya Tabora – Ulyankulu imekuwa sasa ni muda mrefu zaidi ya takribani miaka kumi imejengwa kilometa mbili tu za lami. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana mkakati gani sasa wa kuhakikisha barabara hiyo ya muda mrefu inakwisha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Munde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa Serikali imeshaonyesha nia na kama nilivyosema kwenye baadhi ya majibu yangu kwamba dhamira ya Serikali ni kuzijenga hizi barabara na tumeshaanza, lakini kuikamilisha barabara hii kwa kweli lazima tuseme itategemea na upatikanaji wa fedha. Pale fedha itakapopatikana basi Mheshimiwa Mbunge hii barabara tutaikamilisha kwa kiwango cha lami kama tulivyoahidi na kama tulivyoanza kujenga hizo kilometa za awali. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge twende kwenye swali la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda Mbunge wa Kigoma Mjini.

Na. 9

### **Maboresho Usafiri wa Reli Kigoma-Dar es Salaam**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kuboresha usafiri wa reli ya Kigoma-Dar es Salaam ambao unafanya safari mara mbili kwa wiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-



Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Shirika la Reli Tanzania (TRC) linafanya safari mbili kwa wiki kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na hii ni kutokana na uhaba wa mabehewa ya abiria. Ili kuondokana na changamoto ya upungufu wa mabehewa, Shirika lilianza taratibu za kukarabati mabehewa 37 ambapo mwezi Juni, 2021 ulisainiwa mkataba wa ununuzi wa vipuri kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa hayo. Vipuri hivyo vinatarajiwa kuingia nchini mwishoni mwa mwezi Aprili, kwa maana ya mwaka 2022 na mara vitakapowasili kazi ya ukarabati itaanza. Kazi hiyo ya ukarabati inatarajiwa kufanyika kwa muda wa miezi nane hadi Desemba, 2022 kupitia mafundi wetu wa ndani.

Aidha, Shirika limesaini Mkataba wa ununuzi wa mabehewa mapya ya abiria 22. Mabehewa hayo yanatarajiwa kuingia nchini mwezi Septemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda pamoja na wananchi wa Kigoma kuwa na subira wakati Serikali inaendelea na zoezi la ukarabati na ununuzi wa mabehewa ya abiria. Baada ya utekelezaji wa kazi hizo, idadi ya safari za treni kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma zitaongezeka kutoka safari mbili hadi nne kwa wiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE.KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa hatua ambayo inachukua, hata hivyo ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, uzoefu unaonyesha kwamba wanaponunua mabehewa mapya wanayapeleka katika *route* nyingine na *route* hizo mabehewa yaliyochakaa huko ndiyo wanayaunga kwenye *route* ya Kigoma. Sasa nataka *commitment* ya

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Serikali kwamba mabehewa haya 22 mapya yatakayokuja yatawekwa kwenye *route* hii?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa sababu mabehewa yanayokarabatiwa ni 39 na mapya ni 22 jumla ni mabehewa 59 na bado ni machache na ukizingatia kwamba Serikali ina mkakati wa kuhama kutoka kwenye *narrow gauge* kwenda *standard gauge*; je, Wizara ina mpango wa kukarabati mabehewa zaidi ili yaweze kutumika badala ya kununua mapya ambayo tukianza *standard gauge* tutayaacha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shaban Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anataka kujua *commitment* ya Serikali kwamba mabehewa hayo 22 mapya je, yatakwenda Kigoma. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mabehewa haya 22 yenye thamani ya zaidi ya dola za Kimarekani milioni 14.9 yatakwenda Kigoma na namwalika siku yatakapofika nchini Septemba mwaka huu awe sehemu ya kuyapokea haya mabehewa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, anasema reli inayotengenezwa ni ya *standard gauge* na tuliyonayo ni ya *meter gauge* tunaonaje kwamba hizi reli ziweze kufanya kazi kwa pamoja, lakini pili ziendane na uhitaji wa mabehewa tuliyonayo. *Turn worksheet* ya Mheshimiwa Mbunge kwamba reli ya sasa ya *meter gauge* ina *meter* moja na *standard gauge* ina *meter* 1.475 kwa namna yoyote ile reli tuliyonayo tutaendelea kuitumia hadi hapo itakapokuja kukamilika ya *standard gauge*. Hata ikikamilika, lakini bado hii pia tutaendelea kuitumia. Kwa maana hiyo bado tutaendelea kukarabati mabehewa tuliyonayo kwa sababu *tender* ya kutangaza kutoka Tabora kwenda Kigoma ili ijengwe

*standard gauge* bado itachukua muda. Kwa hiyo bado tutaendelea kutumia ya *meter gauge*. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sebastian Kapufi swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Reli ya Kaliua – Mpanda ni mbovu na ndiyo maana inasababisha mabehewa nayo kuwa mabovu Serikali inasema nini katika hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli reli ya kutoka Kaliua – Mpanda ina changamoto, lakini kama Serikali kupitia shirika letu la reli nchini kila mwaka tumekuwa tukitenga fedha kwa ajili ya kukarabati reli hii. Pia habari njema ni kwamba Mheshimiwa Rais ameridhia kwamba kitangazwe kipande hiki cha Kaliua - Mpanda mpaka Karemi ili kiwe *standard gauge*. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. (Makofi)

Waheshimiwa tumalizie swali la mwisho Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 10

**Udhibiti wa Wanyamapori - Simiyu**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fidia kwa Wananchi wa Simiyu wanaopakana na Hifadhi za Wanyamapori na kuathiriwa na wanyama hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori wa mwaka 2020/2021 mpaka 2025 kwa kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikufanya doria za mara kwa mara kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, Mheshimiwa Rais alielekeza vijengwe vituo vya askari katika maeneo ya Busega na Meatu. Mchakato wa ujenzi umeanza ambapo vituo viwili vitajengwa katika maeneo tajwa mwezi Aprili, 2022. Sambamba na hilo, maombi ya vibali vya kuajiri askari 600 yameshawaliwa kwenye mamlaka husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Simon Mjika.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kushukuru sana...

**SPIKA:** Ahaa hajamaliza kusoma. Samahani hajamaliza kusoma majibu.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Sawa.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni kutoa mafunzo ya mbinu za

kujilinda na kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Jumla ya Halmashauri 17 zimepatiwa mafunzo hayo. Aidha, Wizara ina namba maalum za simu kwenye kila kanda za kiutendaji ili kuwezesha wananchi kutoa taarifa za matukio ya wanyamapori bila malipo.

Mheshimiwa Spika, malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya Sh.790,721,500 imetolewa kwa wananchi 3,598. Aidha, Wizara imepokea maombi ya malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi kutoka wilaya mbalimbali zikiwemo Wilaya za Mkoa wa Simuyu. Kwa sasa Wizara inafanya uhakiki wa maombi kabla ya malipo kufanyika. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Minza Simon Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali langu ni moja tu la nyongeza. Je, ni lini malipo hayo yataanza kwa sababu yamechukua muda mrefu sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maombi tayari tumeshayapata na Serikali imeanza kuyahakiki na kabla ya kuisha mwaka huu wa fedha 2022 wananchi hawa watakuwa tayari wameshalipwa.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na sasa nilete matangazo ya wageni waliopo hapa Bungeni; kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Shamsi Vuai

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nahodha ambaye ni mke wake Bi. Asha Nahodha, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaye ni rafiki yake kutoka Chuo cha SUA Ndugu Dayi Magazine, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ambaye ni mtoto wake ndugu Rukia Haji Ussi kutoka Kusini Unguja ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tawi wa CCM Bungi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 52 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Makanisa ya Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wanamaombi hao Ndugu Isaya Njendaluzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 43 wa Mheshimiwa Ritta Kabati, ambao ni Wanakwaya kutoka Usharika wa Nkuhungu Jijini Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Kiongozi Jacob Ngiliule, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambaye ni Mwenyekiti wa Vijana, Mkoa wa Shinyanga Ndugu Baraka Shemahonge, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na hapa tunaye mgeni mmoja ambaye ni Ndugu Abednego Ibrahim Salilah kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge kama tulivyokubaliana jana, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mara baada ya kuahirisha hapa Shughuli za Bunge Waheshimiwa Wabunge tuelekee Ukumbi wa Msekwa ambako kutakuwa na taarifa ya uchunguzi wa kitaalam wa kuchafuka kwa maji ya Mto Mara na kusababisha kufa kwa samaki itakayotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na yeye atakuwa hapo na

timu yake ya watalaam. Lengo letu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge mpate uelewa kuhusu matokeo ya uchunguzi huo na kama mnayo maswali ya kuuliza basi mpate fursa hiyo ya kuuliza, halafu mtakuwa mmefahamu ni kitu gani ambacho kimefanywa na watalaam wetu.

Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe mambo mawili; la kwanza, niliona hapa Wabunge na hata sasa nawaona kuna Wabunge wanatembea wengine wamesimama mimi nikiwa nimesimama. Nikiwa nimesimama Wabunge mnapaswa kuwa mmekaa. Nadhani hilo limeeleweka, kwahiyo usikimbilie ndani ukishaona Spika amesimama wewe simama huko huko nje maana kuna wengine wakawa wanakimbia ndani kama ndiyo anawahi maana yake ni kwamba umeshachelewa kwa hiyo subiri tu tukishamliza kuzungumza hapa ndani wewe utaingia. Hilo nadhani pia limeeleweka. *(Makofi)*

Maswali Waheshimiwa Wabunge leo tumevuta muda kidogo kwa sababu tulikuwa tunatengeneza mazingira ili watu waelewe namna tutakavyokuwa tunaendesha vipindi vya maswali na majibu. Kwa hiyo leo Wabunge wengi mmepata fursa ya kuuliza maswali, lakini fursa hizo hazitakuwa nyingi kiasi hicho kwa sababu kipindi hiki cha Bunge, muda wa maswali kwenye kipindi hiki cha Bunge la Bajeti ni saa moja. Kwa hiyo asije akakaa hapa Mwenyekiti mkaanza mbona Spika tulizungumza muda mrefu, maswali yalikuwa mengi, hapana. Muda ni saa moja na kwa sababu kuna kuwa na hoja mbele yetu zile hoja lazima zipate muda. Yote ni kazi yetu na lazima yote tuifanye kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Kwa hiyo nimeona niwakumbushe hilo kwamba muda wa maswali ni saa moja, kwa hivyo tutajitahidi kuwapa wengi maswali kwa sababu muda kama mlivyoona hapa, Manaibu Waziri wamejitahidi kujibu maswali yenu ya nyongeza kwa kifupi na ninyi mmejitaahidi kuuliza maswali kwa kifupi. Nilikuwa naangalia muda hapa Wabunge wengi maswali yenu ya nyongeza yaliyoulizwa ukiacha wale wenye maswali ya msingi yameulizwa kwa sekunde kati ya ishirini mpaka

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

thelathini. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge nawapongeza sana kwa hatua hiyo ambayo mmefikia. (*Makofi*)

Pia Waheshimiwa Manaibu Mawaziri pia nao wamejibu kati ya sekunde thelathini mpaka dakika moja, hakuna aliyezidi hapo. Kwa hiyo nawapongeza sana kwa hatua hii tuliyoanza nayo leo, naamini Wabunge wenyewe watakuwa wameona namna ambavyo wanapata fursa nyingi zaidi wakiuliza maswali kwa kifupi na pia kutoa fursa kwa Wabunge wengi kupata nafasi hiyo. Kwa hiyo nimeona niwakumbushe hayo Waheshimiwa Wabunge.

Sasa kwa sababu ya yale ambayo tulizungumza jana Mwezi wa Ramadhani umeanza, kwa hiyo kwa kanuni zetu hatutaweza kukutana kama ilivyo ada. Kwa hivyo nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayesimamia Sera, Bunge na Uratibu awasilishe hoja ya kutengua kanuni.

### HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 34(2) na ya (4) Bunge linakutana hadi saa saba mchana na kusitishwa mpaka saa kumi na moja jioni na baada ya hapo Bunge huendelea kukaa mpaka saa moja na dakika arobaini na tano usiku ambapo Spika husitisha shughuli na kuliahirisha hadi siku nyingine;

Na kwa kuwa Mkutano wa Saba wa Bunge umeanza leo wakati waumini wa dini ya Kiislamu tayari walishaanza Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambapo katika kipindi hicho cha mfungo hutakiwa kuswali na kufuturu kila siku ifikapo saa kumi na mbili na nusu jioni;

Na kwa kuwa ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake zilizopangwa kikamilifu na kwa wakati huo huo kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge ambao ni waumini wa dini ya Kiislamu kuswali na kufuturu kwa wakati muafaka kwa mujibu wa taratibu za dini yao na vilevile kutoa muda



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa kutosha kwa Shughuli za Bunge zilizopangwa, Kamati ya Uongozi iliyokaa jana tarehe 04 Aprili, 2022 ilikubali kanuni ya 34(2) na kanuni 34(4) ya kanuni za kudumu za Bunge zitenguliwe.

Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Shughuli za Bunge wakati huu wa Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani moja; kanuni ya 34(2) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litakutana hadi saa saba mchana ambapo Spika atasitisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa kumi na moja jioni itenguliwe na badala yake Bunge linapositishwa saa saba mchana lirejee saa kumi alasiri badala ya saa kumi na moja jioni.

Mheshimiwa Spika, mbili, kanuni ya 34(4) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litaendelea kukaa hadi saa moja na dakika arobaini na tano usiku ambapo Spika atasitisha shughuli na kuliahirisha hadi kesho yake, itenguliwe na badala yake Bunge liahirishwe ifikapo saa kumi na mbili jioni.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utatumika katika kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na baada ya Mfungo huo kukamilika Bunge litarejea katika utaratibu wake wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

Sasa kwa utaratibu wa kanuni yetu ya 92 nitawahoji kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ya kutengua kanuni (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutengua kanuni hii na mimi kuwahoji maana yake hoja hii imepita kwa hivyo Bunge tutakuwa tukikutana saa tatu asubuhi mpaka saa saba kamili mchana, lakini tutarejea saa kumi kamili jioni ama alasiri mpaka saa kumi na mbili jioni na utaratibu ule wetu wa kawaida utarejea baada ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwisha.

Kwa muktadha huo, siku ya leo kwa sababu mnafahamu kwa utaratibu wetu wa kikanuni ili hoja iweze kusomwa hapa mbele hasa hizi za makadirio ya mapato na matumizi lazima iwe imewekwa Mezani ndiyo ije isomwe, leo imeweka hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hivyo kesho ndiyo tutaanza nayo ili Wabunge waweze kujua nini kilichowekwa hapa mbele.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.00 asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 6 Aprili, 2022, Saa Tatu Asubuhi)*